MTOTO YATIMA
NA
ANAYEISHI KATIKA
MAZINGIRA MAGUMU
(OVC/MVC)
NA
MAHITAJI YAKE

Matumaini Mapya
P. O. Box 1863, BUKOBA/Tanzania
Tel/ Mob: +255 754 678437/ 783 500 905
Email: kagde2009@yahoo.com; info@matumainimapya.or.tz

SURA YA KWANZA

1. UFAFANUZI WA WATOTO YATIMA NA WATOTO WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU

Karibu jamii zote Tanzania zina watoto yatima na watoto walio katika mazingira magumu. Lakini kila jamii ina njia zake za kuwatambua au utaratibu mzuri wa kuwahudumia ambao hauna changamoto.

Watoto walio katika mazingira magumu pamoja na walezi wao walikuwa wakitumia mbinu na njia mbalimbali za kujihami katika kutafuta suluhisho la shida zao.

Mbinu na njia hizi ni zipi? Zingine zikiboreshwa zinaweza kuwa endelevu kwa kutumia vigezo vya kuwatambua watoto walio katika hali ngumu ya maisha pamoja na yatima.

Uundaji wa Kamati za kuongoza shughuli hii ya utekelezaji na usimamizi wa mipango yote ya kusaidia watoto yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ni muhimu kwani tathmini ya makubaliano ya shughuli zote itafanywa na jamii ambayo Kamati zitakazoongoza zimechaguliwa miongoni mwa jamii hiyo.

Utoaji wa taarifa juu ya shughuli nzima za Kamati na jamii kwa ujumla kwa watoto yatima na watoto walio kwenye mazingira magumu ni jambo muhimu sana. Uelewa mzuri wa kutoa taarifa kwenye mashirika husika (NGOs) na wahisani, pamoja na ufuatiliaji mzuri wa mipango yote, mambo yanayohitajika kufanywa mara kwa mara kabla ya kuanzisha mipango mingine kutaweza kuboresha na kutia moyo wanaotoa misaada hiyo na kuiendeleza bila kuisitisha.

Watoto waishio na Virusi vya Ukimwi wanatakiwa kusaidiwa. Kamati zinapashwa kutoa ushauri na kutia moyo wazazi/ walezi wao ili wapate kuwa wanahudhuria kliniki kwa ajili ya kupata ushauri kutoka kwa wataalamu jinsi watakavyoendeleza maisha ya watoto hao. Kusudi hao wenye majukumu na wajibu kutoka ngazi mbalimbali waweze kuwa wanapata kutoa taarifa zilizo sahihi ambazo zitawawezesha walengwa kuishi pamoja na kuendeleza maisha yao yenye matumaini. Na kuzidi kuelewa mjane, matatizo yake, na ushauri anaouhitaji kupata

2. VIGEZO VYA KUWATABUA WATOTO YATIMA NA WATOTO WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU NA MAHITAJI YAO.

S/N	AINA	VIGEZO	ZANA
1	Hali ya Afya	- Kukamilisha chanjo kwa wakati unaotakiwa - Magonjwa yanayowapata watoto mara kwa mara - Wazee/ walezi wa watoto ni wagonjwa muda mrefu	- Kadi ya kliniki - Kumwendea daktari - Taarifa ya afya na mahojiano
2	Hali ya makazi	- Ukubwa wa nyumba kulingana na idadi ya wanaoitumia - Usafi wa mazingira - Choo pamoja na utumiaji wake	- Kuona - Kuona - Kuona
3	Elimu	- Uandikishwaji shule umri wa miaka 7 - Mahudhurio	- Tarifa za shule - Mahojiano na walimu
4	Hali ya lishe	- Uzito wa mtoto chini ya miaka 5 - Upatikanaji wa chakula - Idadi ya milo– Aina ya vyakula	- Kadi ya kliniki - Kuwa na mahojiano - -do-
5	Hali ya watoto wenye ulemavu	- Aina ya ulemavu, kiwango cha ulemavu - Upatikanaji wa huduma kulingana na mahitaji ya msingi/ kijamii - Mtazamo wa jamii kuhusiana na ulemavu huo	- Kuona - Mahojiano - Mahojiano
6	Hali ya mavazi na malazi	- Mavazi yanayoendana na hali ya hewa - Hali ya mavazi yakoje	- Kuona - Kuona
7	Hali ya mlezi/ wazazi	- Umri wa mlezi - Uwezo wa kiuchumi na kijamii/ kipato - Elimu ya mzazi na uhusiano wa mtoto - Idadi ya watoto anaolea, wake na wasio wake	- Kuona/ mahojiano - Kuona/ mahojiano - Kuona/ mahojiano - Kuona/ mahojiano
8	Ajira kwa watoto	- Umri wa mtoto - Aina ya ajira - Namna ya kazi inavyoathiri maendeleo ya mtoto/ watoto - Malipo ya ajira hiyo	- Kuona - Mahojiano - Mahojiano - Mahojiano
9	Hali ya unyanyasaji	- Matukio / Vitendo vya unyanyasaji - Aina ya unyanyasaji - Hatua zinazochukuliwa - Anavyoonekana	- Mahojiano - Majadiliano katika vikundi - Kuona
	MUHIMU	Ikumbukwe pia kuwa si lazima vigezo vyote vitumike. Hata viwili vyaweza kutosha wahusika/ washiriki wasiame wenyewe	

SURA YA PILI

3. NJIA ZA KUKABILIANA NA MAZINGIRA MAGUMU YA WATOTO YATIMA NA WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI.

3.1 **Watoto**

- Kujitafuatia ajira na vibarua mijini na kwenye mashamba
- Kuafanya biasha ndogo ndogo
- Watoto wa kike kuingia kwenye biashara ya mapenzi
- Kuwa ombaomba
- Kujilea wenyewe
- Kuuza vitu walivyoachiwa na wazazi wao au ndugu zao
- Watoto wakubwa kuwalea wadogo zao.
- Kuanzisha miradi midogomidogo ya uzalishaji mali

3.2 **Familia/ Walezi**

- Kugawana watoto miongoni mwa ndugu
- Kutengemea msaada kutoka kwa ndugu wanaoishi mbali (labda wanakipato kikubwa zaidi)
- Kufanya biashara ndogo ndogo
- Kutumia watoto kufanya biashar ndogo ndogo
- Kusukuma watoto kuingia katika ajira kwa lengo la kuleta mahitaji ya familia
- Ufugaji mdogo mdogo
- Kutafuta huduma za kiafya kwa waganga wa jadi badala ya hospitali

3.3 **Jamii**

- Kuwatambua watoto walio katika hali ngumu/ mazingira magumu ya maisha
- Kubainisha matatizo yanayowakabili watoto
- Kutoa misaada kulingana na matatizo yao
- Kuomba misaada nje ya jamaa zao kama NGOs, wafadhili n.k
- Kuwa na Kamati za ufuatiliaaji toka ngazi za chini hadi taifa (ikiwa zimeundwa)

3.4 **Wengine: Azaki, serikali na mashirika ya dini**

- Mashirika ya dini kujitolea
- Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kujitolea kutoa misaada pakiwemo mafundisho/ semina kwa jamii zinazohusika na zisizohusika kupata ufahamu na ugumu wa mazingira waishimo walengwa
- Miradi ya kuongeza pato kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu
- Kulipia gharama za elimu kama karo, sare za shule, madaftari, kalamu michango mbalimbal ya shule n.k

3.5 **Mikakati na njia zinazostahili kuendelezwa**

- Kuwa na Kamati za ufuatiliaji wa watoto hao kutoka kwenye mashirika ya dini au mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kwa lengo la mipango yote inayopangwa na mashirika hayo ya kusaidia na kuboresha maisha ya watoto kama inafanyika au hafanyiki kulingana na jinsi ilivyopangwa
- Kuanzisha miradi midogo midogo ya kusaidia watoto hao kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi
- Mipango endelevu ya malezi ya watoto walio chini ya miaka 5 ili kuhakikisha mambo yafuatayo:
  a. Walezi na wazee wanasaidiwa kupeleka watoto wao wakachanjwe
  b. Kupewa lishe bora
  c. Na mahitaji mengine

4. **MAAMUZI YA KUWEKA VIPAUMBELE VYA UFUMBUZI WA MATATIZO YA WATOTO YATIMA NA WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU**

TATIZO	SABABISHO	UFUMBUZI
Kukosa malazi	- Wazazi kuwajibika ipasavyo (wenye kipato) - Elimu duni ya walezi - Walezi ni wazee hawana uwezo - Ulevi uliokithiri - Umaskini uliokithiri hasa ndani ya jamii	- Elimu ya malezi kwa wazazi (yaani uhamasishaji) - Kuwajengea nyumba walezi wa watoto - Msaada wa nguo n.k - Kuwashauri - Kuwasaidia

MUHIMU: Ikumbukwe kuwa tatizo moja linaweza kuwa na sababisho na ufumbuzi zaidi ya mmoja kwa vigezo mbalimbali. Raslimari zipi ziko kwenye jamii? Utaalamu, ufundi uliopo katika jamii na uwezo wa utekelezaji mipango shirikishi

Pawepo mipango shirikishi kwa jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, yaani NGOs mashirika ya dini zote kufuatana na taratibu za sehemu yalipo kwa ajili ya kulea, kutunza, kulinda na kuhudumia watoto walio katika hali ngumu zaidi.

Baada ya vipaumbele vya matatizo kuonekana, linalobaki ni kuandaa mipango shirikishi kwenye serikali, jamii, mashirika ya dini (makanisa nu misikiti), yasiyo ya kiserikali na ya kiserikali ambayo yako karibu na walengwa ili watoto wapate kuhudumiwa.

Kujadili na kukubaliana yale ambayo serikali na mashirika yake, jamii, mashirika ya dini na ya azaki wameamaua kuyatekeleza katika kusaidia watoto hao. Walezi wa watoto wawezeshwe na wasaidiwe na wataalamu kutoka NGOs husika au serikalini kuandaa mipango ya kulea, kutunza, kulidana na kuhudumia watoto walio kwenye mazingira magumu.

Mipango yote iandaliwe na viongozi na washiriki ambao watakuwa watendaji wakuu wa shughuli za watoto hao kwa kufuata ushiriki wa jinsia na rika zote, wakiwemo watoto wenyewe ili kuhakikisha kile watakachotendewa kinawapa furaha ya utatuzi wa mazingira magumu waliyonayo. Aidha, hii itawahakikishia kwamba jami waishimo bado inawathamini mbali na maisha magumu zaidi walio nayo.

SURA YA TATU

5. UUNDAJI WA KAMATI HUSIKA

Ni vizuri zaidi kuunda Kamati kila sehemu husika ya walengwa na kila Kamati kuipa mipaka yake ya kuhudumia bila kuingiliana.

Kwa kuwa Kamati zitakuwa zimeundwa tayari ingefaa zenyewe ziwe viongozi katika shughuli hii. Na isisitizwe kwamba uandaaji, utekelezaji, usimamizi na thathimini ni juu ya washiriki wenyewe kutoka jamii, makanisa na misikiti. Na kama kuna wataalamu humohumo wanatakiwa hao kutoa ushauri pamoja na kuainisha raslimali zitakazoweza kupatikana wakati wote kwa ajili ya kuwasaidia watoto walio katika mazingira magumu

6. NGUZO ZA MIPANGO SHIRIKISHI

- Pawepo ushiriki changamfu wa washiriki kutoka jamii wote kwa wakati wote wa mchakato wa kuandaa mipango shirikishi ya ndani yao.
- Kuwepo kwa ushiriki wenye uwiano kijinsia katika mchakato mzima wa kuandaa mipango shirikishi
- Maswala na matatizo ya watoto walio katika mazingira magumu zaidi yapewe kipaumbele

7. UMUHIMU WA MIPANGO SHIRIKISHI KUTOKA JAMII, MASHIRIKA YA HIARI MAKANISA NA MISIKITI

Katika kuweka mipango shirikishi kila Kamati pamoja na washiriki waweke lengo kuu ambalo litakuwa la muda mrefu. Weka lengo la muda mfupi na lengo mahususi.

Weka na fursa kufuatana na matembezi na majadiliano ya nyuma, vikwazo, visababishi na ufumbuzi wake (Tazama Jedwali) kutokana na kipindi cha kuweka vipaumbele

- Jadiri hatua za kuchukua ili kukamilisha ufumbuzi
- Je wahusika ni wakina nani?
- Washiriki wote wakubaliane ni kina nani watahusika?
- Mahitaji ni yapi?
- Wawezeshwe washiriki wote kukadiria gharama zote halafu ijulikane ni gharama zipi zitakazotoka kwa jamii, washiriki wa tasisi mbalimbali? Au zipi gharama zitakazotoka nje na ni wapi?
- Je mpango huu au shughuli inayohitaji kufanyika itachukua muda gani?
- Je washiriki watajuaje kuwa mpango huu uliopangwa umefanikiwa au haukufanikiwa?
- Ikiwa haukufanikiwa visababishi au kisababishi ni kipi kipate kutatuliwa.

Muhimu: Kila mipango iwekwe wazi ndipo mafanikio yatapatikana.

SURA YA NNE

8. NAMNA YA KUTOA TAARIFA KWENYE MASHIRIKA HUSIKA NA WAHISANI

8.1. **Watoto walio katika mazingira magumu**

- Idadi ya watoto walio katika mazingira magumu zaidi waliokwishatambuliwa na jamii, serikali, makanisa au misikiti na wangapi ni
  i) Wavulana?
  ii) Wasichana?
- Kaya zote zenye watoto walio katika mazingira magumu ni ngapi?
- Idadi ya watoto wote wakiwa kwenye mafungu
  i) Miaka 0-5 Me Ke
  ii) Miaka 5-13 Me Ke
  iii) Miaka 14- 18 Me Ke

S/N	UMRI (Miaka)	ME	KE
1	0-5		
2	5-13		
3	14-18		
	JUMLA		

8.2 **Hali ya elimu**

S/N	AINA YA SHULE	ME	KE
1	Chekechea		
2	Shule za awali		
3	Shule za msingi		
4	Shule za sekondari		
5	MEMKWA		
6	Vyuo		
7	Hawakuandikishwa		
	JUMLA		

- Zoezi hili ni muhimu likafanyika kila baada ya miezi mitatu.
- Idadi inaweza kuongezeka au kupungua kutokana na vifo au wazazi kuhama

8.3 **Nyongeza kwenye taarifa**

Toa taarifa ya mzazi/ mlezi kama ifuatavyo:- Jina la kijiji/ mtaa, kata, jinsi,

- **Umri wa mzazi/ mlezi yakiwa kwenye mafungu 3**

S/N	UMRI (Miaka)	KE	ME
1	Chini 18		
2	18-60		
3	60 zaidi		
4	Idadi ya wategemezi		
	JUMLA		

9. UMUHIMU WA UFUATILIAJI WA MIPANGO YA KAMATI ZA JAMII, MAKANISA NA MISIKITI

Inafaa mipango shirikishi itekelezwe kwa wakati uliopangwa na kamati husika. Wawezeshaji ambao ndiyo Kamati toka mwanzo waonyeshe kuwa tatizo/ matatizo ya watoto walio kwene mazingira magumu au zaidi pamoja na watoto yatima ni wa jamii yenyewe.

Serikali yenyewe ni kutia chachu katika utekelezaji wa mipango endelevu ya jamii, watathmini na kutambua ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wataalamu walionao au wawezeshaji kutoka kwenye NGOs husika

Kila mwanakamati husika afanye sehemu yake aliyopangwa bila maingilaiano na mtu mwingine hata sehemu ile ikiwa wapo jamaa na rafiki zako, usiishughulikie kuvuka mpaka wako. Na kamati nzima vilevile isivuke mipaka yake inayoishughulikia kwa ajili ya kulinda amani na kuwa na uhakika wa kile kinachofanyika.

Kama utekelezaji utahitaji fedha, basi udhibiti bora wa matumizi ufanywe kwa ajili ya kulinda uaminifu wa Kamati na kufanya wale wanaochanga au utoaji wa fedha za kuwasaidia watoto yatima na watoto walio kwenye mazingira magumu na

magumu zaidi kuwa na uhakika wa fedha zao kuwa zinafanya kile kilichokusudiwa.

Muhimu: Kila kazi au mipango yote inayaofanyika sharti itolewe nakala na kupelekwa kwenye ofisi ya mashirika husika au kwa wahisani wote wanotoa fedha kugharamia mipango yote ya kusaidia watoto yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na magumu zaidi. Hii itasaidia kuwatia moyo wa kuzidisha michango ya fedha zao kwa ajili ya kufanikisha zoezi hili. Wanakamati wanapashwa kuandaa ratiba ya utekelezaji, ufuatiliaji na thatmini ya mipango yao, kufuatilia na kuangalia viashiria ambavyo vitakuwa vimewekwa kwa muda maalumu.

10 FAIDA NA UMUHIMU WA UFUATILIAJI

Ufuatiliaji lazima uambatane na kuzingatia haya yafuatayo:-

a) *Mafanikio*
- Je, washirika katika jamii wamefanikiwa nini katika kutatua matatizo ya watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu na magumu zaidi?
- Je washiriki hao watajuaje au kuelewa ni jinsi gani walivyofanikiwa katika utekelezaji na vipi wamefanikiwa katika mipango yao?

b) *Kupima maendeleo*
- Je malengo yaliyowekwa yamefikiwa?
- Je washiriki wanafanya yale waliyokubaliana?

c) *Ufuatiliaji*
- Je mipango inakwenda vizuri?
- Je wahusika wanafaya yale waliyopangiwa?

d) *Mapungufu na mema*
- Je mipango imefanikiwa vizuri au inaweza kurekebishwa.
- Je malengo ya kwanza bado ni bora au yanahitaji kubadirishwa?
- Je watoto walio kwenye mazingira magumu zaidi wanaongezeka au wanapungua?
- Je yale matatizo yanapungua au yanazidi kuongezeka?
- Je, lishe ya watoto inaboreka?
- Je, Elimu ya watoto inaendelea vizuri
- Je uwezo wa kaya unaongezeka au unapungua?
- Je, mwamko wa washiriki ambao ni uti wa mgongo wa walengwa wanaoishi pamoja unaongezeka au unapungua?
- Je, ikiwa mwamko unapungua unasababishwa na nini?
- Je mpango upi unaoweza kufanyika ili kuwarushishia mwamko huo?
- Je vifo vya watoto yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na magumu zaidi vinapungua au vinaongezeka?

e) Je gharama zilizokadiriwa na zilizotumika ni sahihi na zinalingana na matokeo au hazilingani na matokeo?

f) Ikiwa hazilingani na matokeo zinasababishwa na nini kutolingana na mipango iliyokusudiwa?

g) Je taarifa zinazotolewa na mashirika na wadau husika pamoja na wahisani zinakuwa sahihi au sio sahihi

h) Ikiwa taarifa sio sahihi kwa nini zinatolewa?

i) Je, washiriki katika jamii wanayo mambo ya kujituma kutoka kwenu au kubadirisha na kuboresha?

Mwisho: Mafanikio ya mipango yote ya kuleta maendeleo yanatokana na ufuatiliaji bora. Bila ufuatiliaji ulio bora wa mipango na uboreshaji hakuna mafanikio yanayoweza kujitokeza

Mkazo: Wanakamati katika jamii, makanisa na misikiti msikose kufanya ufuatiliaji wa mipango yenu kusudi mafanikio yapate kuonekana. Maswali yaliyotajwa yote yanatakiwa kuulizwa swali moja hadi jingine ikiwa ni tathimini ya ufuatiliaji wenu. Mahali mnapokuta dosari sahihisha kwa vitendo sio kwa maneno na maandishi

11 UUNDAJI WA KAMATI

Pawemo kwenye Kamati zitakazoundwa watu wafuatao:

- Mwenyekiti
- Katibu
- Mweka hazina
- Yatima mmoja
- Mtoto aliye kwenye mazingira magumu
- Baba mmoja (k.m. mgane)
- Mama mmoja (k.m. mjane)

Uchaguzi ufanywe kufuatana na jinsia. Pasiwepo upendeleo wa jinsia moja

Na.	**Sifa za kila mwanakamati**
1.	Asiwe mlevi au mzinzi
2.	Ajue kutunza siri
3.	Awe mwaminifu
4.	Asiwe mpenda au mla rushwa
5.	Mwenye kupenda kusaidia wengine
6.	Kuwa na ushuhuda mzuri
7.	Anayekubalika kwenye jamii anamoishi
8.	Aliyetayari kusikiliza shida
9.	Ana ufahamu mzuri
10.	Anayekuwa tayari kukosoa na kukosolewa
11.	Anayejua kusoma na kuandika vizuri
12.	Awe mtu mvumilivu
13.	Awe mtu mwenye roho ya kutosheka
14.	Asiwe mwenye tama
15	Awe tayari kuitikia na kutumika wakati unaofaa na usiofaa

SURA YA SITA

12 UFAFANUZI WA WATOTO YATIMA, WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI NA WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI

Mtoto yatima

Ni neno linalotumiwa kumuita mtoto yeyote yule aliye na au chini ya umri wa miaka 18 ambaye amefiwa na mzazi mmoja au wote wawili (mwana mkiwa)

13 WATOTO YATIMA NA WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU

- Ni watoto walio chini ya miaka 18 ambao wamefiwa na baba, mama au wazazi wote wawili (baba na mama); watoto ambao wanaishi na, au wanaugua virusi vya ugonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS); watoto wanaoishi

katika familia zilizoathirika na ugonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS) au watoto ambao kwa njia moja au nyingine wako katika mazingira magumu au hatarishi kutokana na umasikini uliokithiri, ugonjwa hatari katika familia, unyanyaswaji na uonevu (PACT)

- Ni mtoto chini ya miaka 18, ambaye anakosa au anaelekea kukosa matunzo na ulinzi wa kutosha (Ustawi wa Jamii-Tanzania).
- Kwa vyovyote vile, haya mambo matatu husababisha watoto kuwa katika mazingira magumu:
  - Kupungua kwa uwezo wa kupambana na majanga
  - Kutengwa katika masuala ya elimu, afya, ustawi, usalama, michezo, ushiriki
  - Kukosekana kwa huduma za matunzo

14 WATOTO WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI

- Ni watoto ambao wameambukizwa ukimwi kutoka kwa wazazi wao, kuzaliwa nao au kuambukizwa wakati wa kunyonya maziwa ya mama zao, au wameabukizwa kutoka nje ya wazazi wao kutokana na mazingira yanayowazunguka, k.m. wakati wa matibabu na huduma za afya, nk.

15 MAKUNDI YA WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI

Utafiti uliofanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto duniani (UNICEF) mwaka 1997/98 ulibainisha kuwa kwenye jamii yapo makundi manane ya watoto walio katika mazingira magumu. Makundi hayo ni kama yafuatayo:-

- Watoto wanaonyanyaswa na kutelekezwa
- Watoto wanaoozwa katika umri mdogo kwa kupata mimba na kuolewa
- Watoto wanaoingia kwenye ajira za nyumbani au ajira za hatari
- Watoto wenye ulemavu
- Watoto wanaoishi mitaani
- Watoto wanofanya biashara ya ngono
- Watoto wanaokinzana na sheria (obstruct = zuia, piga,kinza)
- Watoto wanaouguza wazazi wao kwa muda mrefu

Wengine: Kuna watoto wanaoishi kwenye makao maalum kama:

- Shule ya maadilisho
- Vituo vya mpito (hawapati nafasi ya kujifunza kazi, wanakosa huduma ya kisaikolojia na huduma za msingi (Saikologia- Elimu nafsia)

  - **Saikolojia:** Ni elimu inyohusiana na ufahamu na utendaji kazi wa nafsi au akili ya mwanadamu– elimu ya nafsi

16 MAHITAJI MUHIMU YA WATOTO

Pamoja na haki za mtoto zinazotamkwa katika sheria za nchi, mikataba ya kitaifa na kimataifa, mtoto anayo mahitaji muhimu ili aweze kuishi na kukua na kuwa mtu mzima mwenye uwezo wa kuchangia katika maendeleo ya jamii na nchi yake anamoishi pindi atakapo kuwa mtu mzima.

- **Kimwili**: Chakula, nyumba, malazi, mavazi, huduma za afya n.k.
- **Kijamii**: Usalama, malezi, wazazi, ndugu, michezo, n.k.
- **Kiakili**: Elimu ya nyumbani (mila na desturi- elimu dunia), shuleni (elimu ya kisasa), malezi bora kutoka kwa walimu na jamii inayomzunguka.

- **Kiroho/ saikolojia**: Kuishi na kukua akimjua Mungu wake (kupitia dini), na elimu ya kutambua nafsi.

17 WATOTO YATIMA

Ikumbukwe kwamba yatima anaweza asiwe kwenye mazingira magumu (zaidi), anaweza kuwa amefiwa na mzazi mmoja na wa pili aliyebaki anaouwezo wa kumtunza au kuwatunza watoto waliobaki au kutoka kwenye jamaa ya mama akiwa/ wakiwa wamefiwa na baba au kwenye jamaa ya baba akiwa/ wakiwa wamefiwa na mama wapo wenye uwezo wa kutunza mtoto/ watoto hao.

Yawezekana pia kuwa watoto yatima kutokana na kufiwa na wazazi wote (baba na mama) wasiwe kwenye mazingira magumu kutokana na, pamoja na sababu zilizotajwa hapo juu, wazazi wao waliacha raslimali za kutosha za kuwatunza watoto hao. Watoto wa aina hii sanasana wanaweza kuhesabika kuwa katika mazingira magumu kwa vile wanakosa malezi na mapenzi ya wazazi wao.

Hivyo si kweli kwamba yatima yeyote ni muhitaji kinachotakiwa ni kufanya uchunguzi kabla ya kutoa mahitaji. Kutokana na kukosa uchunguzi wa kina unakuta anapewa mahitaji yatima asiyestahili na yule anayestahili kupewa mahitaji anakosa.

Hitaji muhimu: Uundaji wa Kamati za uchunguzi zilizokaribu na walengwa kutoka jamii, makanisa na miskiti zinahusika sana kutatua matatizo hayo.

18 MIKAKATI NA NJIA ZINAZOSTAHILI KUENDELEZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI ZILENGE MAENEO YAFUATAYO:

a) **Kinga**
- Elimu juu ya Ukimwi
- Upimaji
- Malezi ya wazazi
- Walezi
- Stadi za maisha
- Kuimarisha ndoa (Uaminifu)

b) **Huduma na matibabu ya magonjwa nyemelezi**
- Matibabu ya magonjwa ya ngono
- Kisonono
- Kaswende

c) **Dawa za kurefusha maisha**

d) **Huduma majumbani zinazotolewa na**
- Washauri nasaha
- Washauri majumbani
- Wahudumu wa afya
- Jamii

e) **Misaada** kwa waathirika, watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi, wajane, n.k.

f) **Misaada:** Ipi inayowezakutolewa?
Chakula, nguo, elimu na vitendea kazi vyake, ushauri, msaada wa kiroho, malazi, n.k.

g) **Ulaghabishi (Advocacy)**: Kupiga vita unyanyapaa na unyanyasaji
Haki za watoto
- Kuishi
- Kulindwa
- Kuendelezwa
- Kushirikishwa
- Kutobaguliwa

h) **Kuzuia:** Kuzuia maambukizi toka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto.

19 ATHARI ZA UKIMWI
- Kuongezeka kwa watoto yatima
- Kuongezeka kwa wajane
- Umaskini
- Kupungua kwa nguvu kazi (wataalamu)
- Njaa
- Mabadiliko ya majukumu nyumbani
- Kuongezeka kwa vifo

20. TOFAUTI YA MAHITAJI KULINGANISHA NA WATOTO YATIMA

HITAJI	HALI YA HITAJI	WEKA TIKI	HITAJI	HALI YA HITAJI	WEKA TIKI
Chakula	*Duni*		**Upendo**	*Wastani*	
Malazi	*Duni*		**Kucheza**	*Wastani*	
Mavazi	*Wastani*		**Afya**	*Duni*	
Malezi	*Wastani*		**Huduma za kiroho**	*Duni*	
Elimu	*Wastani*				
Ulinzi	*Wastani*				
Kushirikishwa	*Hakuna*				

SURA YA SABA

21 MAJUKUMU NA WAJIBU WA NGAZI MBALIMBALI ZIHUSUZO MALEZI YA WATOTO YATIMA

Kwa kuwa suala la malezi ya watoto yatima linahusu ngazi mbalimbali za chini hadi kitaifa na kimataifa hapana budi majukumu na wajibu wa ngazi hizo ueleweke vyema. Majukumu na wajibu wa ngazi zote ni kama ifuatavyo:

a) **Ngazi ya familia**
- Kulea watoto yatima
- Kutoa taarifa ya watoto yatima kwa serikali ya kitongoji, kijiji/ mtaa kuhusiana na matatizo kama vile vifo
- Kutoa taarifa ya matatizo yanayowakabili watoto na walezi wao na mahitaji yao

b) **Ngazi za kitongoji, kijiji/ mtaa**
- Kufahamu idadi ya watoto yatima katika eneo lao
- Kutambua mahitaji yao
- Kuoanisha mahitaji yao na raslimali zilizopo
- Kuelimisha jamii juu ya matatizo na mahitaji ya watoto yatima

- Kuandaa na kuendesha harambee za kuchangia misaada kwa watoto yatima
- Kuchukua hatua zinazostahili za malezi ya watoto yatima
- Kutunza kumbukumbu zinazohusiana na malezi ya watoto yatima
- Kuweka utaratibu akiba kutokana na raslimali zilizopo kwa ajili ya watoto/ mtoto yatima
- Kusimamia utekelezaji na uratibu wa shughuli za malezi ya watoto yatima
- Kuandaa takwimu na kutoa taarifa kwenye ngazi ya kata kuhusu mahitaji, maendeleo na malezi ya watoto yatima na watoto wengine kwa ujumla.
- Kuweka utaratibu wa kudhibiti mali na raslimali zilizoachwa na wazazi kwa ajili ya watoto yatima ili zisifujwe
- Kujadiri suala la malezi ya watoto yatima na kuweka mipango na mikakati ya namna ya kupata raslimali kwa ajili ya kuwasaidia watoto yatima.
- Jamii inaposhindwa kupata raslimali za kutosha kwa ajili ya kuwahudumia watoto yatima, iwasiliane na vyombo vilivyopo nje ya jamii kama vile NGOs, CBOs na taasisi zingine zinazohusika na masuala ya watoto yatima ili kupata msaada na ushauri.

c) **Ngazi za kata na wilaya**

- Kupokea na kuhifadhi taarifa na takwimu za waoto yatima kutoka kwenye vitongoji, vijiji/ mitaa; au kata (Ikiwa ni kwenda Wilayani)
- Kuchambua taarifa na mahitaji halisi ya watoto yatima kwa madhumuni ya kuoanisha na raslimali zilizopo
- Kutoa taarifa halisi kuhusu huduma kwa watoto/ mtoto yatima kwenye ngazi ya mkoa na kwa watumiaji wengine wanoitaji taarifa hizo kwa lengo la kuboresha huduma hizo.
- Kuelekeza wale wote wanopenda kutoa huduma za malezi ya watoto yatima kwenye maeneo yanayohitaji misaada kam vile NGOs, CBOs na taasisi nyingine zinazohudumia watoto yatima
- Kutunga sheria ndogo (by-laws) za kulinda maslahi na mali za watoto yatima na kuhakikisha kwamba sheria hizo zinatumika.

22 MAELEZO KUHUSU UTUNGAJI WA SHERIA NDOGO (BY-LAWS) ZA KULINDA MALI ZA WATOTO YATIMA

Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana iliweza kutoa mwongozo na mikakati ya huduma kwa watoto yatima, watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na magumu zaidi mnamo mwezi October 1994 Dar-Es-Salaam.

- Utungaji wa katiba unatoka kwa walezi wa walengwa kufuatana na mila na desturi za mahali pale
- Kuratibu shughuli zote zinazohusu utoaji taarifa/ huduma za malezi kwa watoto yatima katika wilaya
- Kukutanisha wakala za hiari, NGOs, mashirika ya dini na wahisani wanaotoa huduma kwa watoto yatima wilayani, kwa lengo la kubadirishana mawazo na kuweka mikakat ya pamoja ilikudumisha uelewano na ushirikiano

Kumbuka: Kuna majukumu ya ngazi ya mikoa na taifa

23. MAJUKUMU YA WAKALA (NGOS) HUSIKA, MASHIRIKA YA DINI NA WAHISANI

Ni kusaidia watoto yatima na walezi wao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu pamoja na kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na magumu zaidi, watoto wa mitaani kwa kuwapa misaada muhimu inayotakiwa ili kuwajenga uwezo wao kiuchumi, kielemu na kimaisha.

24. MJANE

24.1 **Maana ya Mjane na Mgane**

- *Mjane* ni mwanamke yeyote aliyefiwa na mme wake (awe ni wa ndoa au siyo wa ndoa).
- *Mgane* ni mwanaume yeyote aliyefiwa na mke wake (awe ni wa ndoa au siyo wa ndoa).

24.2 **Uthibitisho wa mjane kulingana na maandiko makatifu**

Kuanzia wakati wa Agano la Kale mwanamke aliitwa mjane wakati alipofiwa na mme wake bila kujali umri.

24.3 **Hali ya mjane alivyokuwa akiishi wakati huo**

Wakati mwanamke aliyekuwa akifiwa na mme wake, katika maisha yake yote alihitajika kuonekana siku zote kuwa ni mjane. Alihitajika kuvaa nguo za ujane kila siku, na kujizuia na tamaa za kidunia. Ikiwa alihitaji kuolewa, na akaolewa na mme mwingine hapo ujane ulikuwa unaisha. Alikuwa haitwi tena mjane bali alibakia kuitwa mke kwa maana amepata mme mwingine.

Wakati wa miaka ya A.D (Baada ya Kristo) mwanamke alipokuwa akifiwa na mme wake kuja kuitwa mjane kweli kweli alihitajika kuwa na sifa zifuatazo:

- Kuwafundisha watoto au wajukuu kumjua Mungu
- Watoto/ wajukuu wakiwa wakubwa ni jukumu lake kuwafundisha na kuwatiisha ili wapate kuwasaidia wazazi na jamaa zao
- Awe mtu ambaye ni mcha Mungu kila wakati
- Awe mtu wa kudumu katika maombi mchana na usiku
- Na awe mtu wa kujizuia na tama za kidunia na mke wa mme mmoja (aliyekufa)
- Awe mtu ambaye anashuhudiwa kuwa na matendo mema.
- Awe mtu ambaye anajua kuwakaribisha wageni na kuwaosha miguu watakatifu na kuwasaidia wateswao na kufuata kwa bidii kila tendo jema
- Muhimu sana awe amefikisha umri wa miaka sitini (60). Huyo ndiye anayehitajika kuhesabika mjane kwelikweli na wa kuheshimiwa

24.4 **Hali ya vifo kwa wakati wa B.C na A.D**

Hali ya vifo vya wakati uli wa miaka ya B.C (Kabla ya Kristo) na miaka A.D (Baada ya Kristo) vilikuwa vya kawaida. Ugonjwa hatari wa UKIMWI ulikuwa haupo

24.5 **Wajane walio vijana**

Wajane walio vijana walikuwa hawakubaliwi kuitwa wajane. Kwenye orodha ya wajane walikuwa wanakataliwa kuandikwa humo. Hata kanisa lilikuwa haliwapi misaada yeyote ila walikuwa wakisaidiwa na waumini waliokuwa wakiishi nao kwa sababu:

- Walikuwa hawahaminiki katika mienendo yao kwa sababu ya kuwa na tamaa
- Walilitia kanisa mashaka ya kuwaita wajane kwa vile wengi wao walipokuwa wakizidiwa na tamaa kinyume mafundisho ya Kristo walitaka kuolewa na kuiacha imani yao ya kwanza.
- Kwa kutojizuia walikuwa wakiyatenda mambo ya aibu

24.6 **Hali ya vifo kwa wakati huu tulionao**

Hali ya vifo kwa wakati huu tulio nao ni vya kutisha sana kwa sababu vifo hivi vinasababishwa na ugonjwa hatari wa UKIMWI. Ugonjwa huu unaua familia nzima bila kubakia mtu yeyote. Ni ugonjwa ambao ni rahisi sana kuenea katika jamii ambayo inashindwa kuchukua hatua za kujikinga kwa kufuata ushauri wa wataalamu. Hivyo vifo vya wakati huu ni zaidi sana kuliko vifo vya wakati ule wa Agano Jipya na Agano la Kale

24.7 **Hali ya wajane kwa wakati huu**

Wakati huu tulionao hatuna ubaguzi wa wajane. Mjane kijana na mjane mzee wote wanahesabiwa kuwa wajane na kuheshimiwa katika ujane wao kwa sababu zifuatazo:

- Kutokana na ugonjwa wa ukimwi ambao umeenea kila sehemu umesababisha vifo vingi kwa familia na hasa za watu wa umri mdogo wa ujana.
- Wajane wamekuwa wengi na yatima wamekuwa wengi mno wanaohitaji kusaidiwa
- Hali ya wahitaji inaongezeka mara kwa mara.
- Hali ya uchumi imekuwa duni sana
- Wakati tulionao hakuna ubaguzi wa umri, dini, jinsia, kabila, n.k. Kinachowekewa kipaumbele ni kuwahudumia wajane kwa kuwapa mahitaji yao. Neno la mungu linasema "Usimtese mjane yeyote aliyefiwa na mumewe, wala mtoto yatima. Ukiwatesa watu hao katika neno lolote, nao wakanililia mimi, hakika yangu nitasikia kilio chao, na hasira yangu itawaka moto, nami nitawaua ninyi kwa upanga; na wake wenu watakuwa wajane, na watoto wenu yatima"

24.8 **Mjane anakuwa na matatizo gani?**

- Upweke wa kukosa mwenzi wa kushirikiana naye katika
  - ✓ Kuwalea watoto
  - ✓ Kuzalisha mali kwa matumizi ya familia
- Kutothaminiwa na jamii anamoishi, na hasa inapotokea kuwa kifo cha mumewe kilitokana na ugonjwa wa ukimwi.
- Kutengwa na ndugu wa ukoo wa mme
- Katika makabila mengine; kulazimishwa kurithiwa (kuolewa) na ndugu wa marehemu, kufanyiwa utakaso n.k.
- Kunyanyapaliwa
- Kunyanyaswa na kunyanganywa mali zake za familia (ndoa)
- Kupungua kwa usalama na ulinzi wake kutoka kwa wanajamii.
- Kuamriwa maswala mengine yanayohusu familia yake bila kushirikishwa

24.9 **Ushauri na msaada gani anahitaji njane?**

- Kumjua Mungu
- Jamaa na familia kutokuwa mbali naye
- Kutambua vizuri kifo cha mme wake
- Kumwelekeza ili awe anapata ushauri wa wataalamu jinsi anavyoweza kutunza afya ya kimwili. Ikiwa ameishaathirika na ugonjwa wa ukimwi jinsi anayoweza kutumia madawa anayoyapata kwa kurefusha maisha yake.
- Pamoja na kupata ushauri wa kiroho kutoka kwa watumishi wa Mungu kama vile Mapadre, Wachungaji, Makatekista, Wainjiristi na Mashekhe wakimtia moyo ili apate kuishi kwa matumaini na kutambua kuwa Mungu

hana ubaguzi hata na yeye bado anampenda ndiyo maana anaendelea kuishi

- Kuwa tayari kueleza kifo cha mme wake na sababu iliyosababisha kifo chake (hata kama ni UKIMWI) bila kuficha hata na watoto wake.
- Kumtuoa hofu na kumuelimisha kwamba madhara ya virusi vya ukimwi hayamuathiri yeye peke yake ila ni kw afamilia nzima ikiwa hawafuati ushauri wa wataalamu; ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuepukana na visababishi vya ukimwi na jinsi ya kujikinga na ukimwi au jinsi ya utumiaji madawa ya kurefusha maisha
- Afundishwe kutolalamika ila awetayari kuomba msaada katika kutatua matatizo yanayomkabili pamoja na kutumia raslimali alizonayo kwenye mazingira yanayomzunguka
- Kwa mjane ambaye mme wake kabla ya kufa walikuwa na miradi inayozalisha mali yenye mapato mazuri. Wakati mme wake anapofariki utakuta naye yuko kwenye msafara wa kuomba unifomu za watoto wake wa shule.
    - ⇒ Mjane kama huyu anatakiwa kupewa ushauri kwamba mahitaji anayopewa yatima siyo tuzo la kuwa **mtoto yatima** bali ni kwa ajili ya kumpunguzia makali ya maisha. Mjane kama huyu anatakiwa kushauriwa jinsi ya kundeleza miradi hiyo isiharibike ili iweze kuwa msaada mkubwa kwa watoto wake ambao ni yatima.

- Kulindwa dhidi ya kunyangaywa mali zilizoachwa na mme wake wakati anapofariki.
    - ⇒ Kuna baadhi ya wanaukoo wa marehemu, na hasa ndugu zake wa karibu na mme wa mjane ambao huingilia kwa nguvu mjane na kunyang'anya mali zote zilizoachwa na mme wake wakidai kuwa ni mali zao. Mjane huachwa na kufukuzwa bila kitu chochote huku wakijua kuwa mali hizo walizichuma wote kwa pamoja.
    - ⇒ Bahati mbaya ikiwa mjane huyo hakubahatika kuzaa pamoja na mme wake aliyefariki, hapo hufikia wakati wa kufukuzwa kabisa na wanaukoo kutoka kwenye mali hizo.
        - ❖ Mjane wa namna hiyo anatakiwa kupewa ushauri wa kuwaendea wakuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii na asasi zinazoshughulikia wajane ili apate kusaidiwa kurudishiwa mali zake. Hata ikiwa mme wake amezirithi kutoka kwa baba yake mzazi, mjane asinyang'anywe mali hizo.